# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI KWA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika,

Kwa heshima kubwa natanguliza shukrani zangu za dhati kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehema kwa kutujaalia sote kuwa na afya njema na kutuwezesha kufika hapa leo kuendelea na shughuli za ujenzi wa taifa letu.

Mheshimiwa Spika,

Kamati inachukuwa fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuipa kipaumbele sekta ya Utalii nchini kwa maslahi mapana ya taifa letu.

Mheshimiwa Spika,

Kamati yangu pia inatoa pongezi zake za dhati kwa Makamo wa kwanza wa Rais, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdallah, kwa kumshauri vyema Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake mazito ya kitaifa

Mheshimiwa Spika,

Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mhe. Simai Mohammed Said Pamoja na timu yake inayoongozwa na Katibu Mkuu, ndugu Fatma Mabrouk Khamis kwa kusimamia vyema

utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Hata hivyo, kwa namna ya pekee naomba niwapongeze wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa kwa jinsi wanavyotekeleza majukumu yao ya msingi katika kuipatia Wizara hii miongozo na ushauri unaofaa katika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Naomba niwatambue wajumbe hao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Yussuf Hassan Idd | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Aza Januar Joseph | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Saada Ramadhan Mwedwa | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Said Saleh Salim | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Jumla ya maagizo 48 yalitolewa na Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii katika kikao cha Februari 2022 kwa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Kiujumla, Kamati imeridhika na utekelezaji wa maagizo hayo, hata hivyo Kamati inaiomba Wizara kuwa makini na mambo yanayotokana na maagizo yafuatayo:

## UCHAKAVU WA MIUNDOMBINU KATIKA MAENEO YA KIHISTORIA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati iliagiza kufanyiwa matengenezo kwa miundombinu ya barabara ziendazo katika maeneo ya kihistoria kufuatia uchakavu mkubwa wa miundombinu hiyo. Ni dhahiri kwamba, maeneo mengi ya kihistoria, miundombinu ya barabara utekelezaji wake bado ni changamoto, kutokana na ukweli kwamba barabara hizo ni mbovu na hazifikiki kwa urahisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa muktadha huu, Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano kuziingiza katika miradi ya maendeleo barabara zote ziendazo katika maeneo ya kihistoria kwa lengo la kuzifanyia matengenezo ya uhakika barabara hizo. Miundombinu hii endapo itatengenezwa, itasaidia katika kuyaimarisha maeneo hayo na kuongeza mvuto kwa wageni wanaoingia katika maeneo hayo, ongezeko la wageni katika maeneo ya kihistoria ni kuongezeka kwa pato la taifa letu.

## HATI MILIKI KWA MAENEO YA KIHISTORIA

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Utalii ni Wizara iliyobarikiwa kuwa na maeneo mengi ya kihistoria ambayo kwa njia moja au nyengine husaidia katika kuongeza pato la taifa wakati ambapo wageni wataingia katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati katika ziara zake, ilibaini uwepo wa changamoto kubwa ya ukosefu wa hati miliki kwa maeneo ya kihistoria, ambapo, Kamati iliiagiza Wizara ya Utalii kuharakisha upatikanaji wa hati hizo kwa kufuatilia kikamilifu katika Wizara husika. Kwa mujibu wa taarifa iliyopokelewa mbele ya Kamati

Wizara ina jumla ya maeneo  ya kihistoria **86** yaliyotangazwa kwa Unguja na Pemba. Kati ya maeneo hayo, maeneo **20** tu ndiyo hadi sasa tayari yameshapatiwa hati hizo, maeneo yote haya ni kwa upande wa Unguja.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa hati hizo kwa yale maeneo ambayo hadi sasa bado hayapatiwa hati hizo, kwa lengo la kuyahifadhi na kuyanusuru na uvamizi unaoendelea siku hadi siku, kufanikiwa kwa hatua hii kutasaidia sana katika kuepusha migogoro kati ya Serikali na wananchi wake.

## SHUGHULI ZA UTALII PEMBA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati iliiagiza Wizara ya Utalii kupitia Kamisheni ya Utalii Zanzibar, kuharakisha zoezi la kuweka vivutio vya Utalii kisiwani Pemba kwa lengo la kuimarisha utalii kisiwani humo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, shughuli za utalii kwa kipindi kirefu zilikuwa hazijaimarika kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ukosefu wa miundombinu ya barabara na umeme.

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali ya awamu ya nane imejipanga kuhakikisha kwamba sekta ya utalii inaimarika katika kisiwa cha Pemba na kukuza uchumi wa Taifa na pato la wananchi kwa ujumla. Ili azma hii ya Serikali iweze kufikiwa, Kamati inaendelea kuishauri wizara ya Utalii kuvitangaza vivutio vipya vya utalii vilivyoibuliwa kisiwani Pemba kupitia vyombo mbalimbali vya habari nchini. Aidha, wizara ijipange katika kuandaa ratiba maalumu ya kufanya matamasha na makongamano yenye lengo la kuifungua zaidi Pemba kiutalii.

## MATUMIZI YA MASHINE ZA KIELEKTRONIKI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati iliagiza Wizara kupitia taasisi zake kuachana na mfumo wa kupokea mapato kwa risti za mkononi na badala yake mfumo wa kielekroniki uchukuwe nafasi katika hili, lengo ni kuzuia upotevu wa mapato hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imeridhika na utekelezaji wa agizo hilo ambapo Wizara imeshaanza kuutumia mfumo huu wa ukusanyaji wa mapato kwa kuweka mashine hizo katika maeneo mbalimbali ya kihistoria yakiwemo Kasri la Kibweni, Mangapwani, Fukuichani na Mtoni.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaendelea kuishauri wizara ya Utalii kuisimamia ipasavyo mifumo hii kuepukana na kuchezewa kwa lengo la kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha za Serikali katika taasisi tunazozisimamia.

## MAPITIO YA SHERIA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati iliiagiza Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuzifanyia marekebisho sheria zote ambazo zinaleta mgongano wa kiutendaji miongoni mwa taasisi zetu. Utekelezaji wa suala hili bado haujawa wa kuridhisha kutokana na Wizara ya Utalii kusubiria msaada wa kifedha kutoka benki ya dunia.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Utalii kujipanga na kutumia vyanzo tofauti vitakavyowezesha kuzifanyia marekebisho sheria zote ambazo zinaleta ukakasi katika utekelezaji wake.Lengo ni kuondosha kabisa migongano ya kisheria miongoni mwa taasisi za Serikali.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali imeamua kuwekeza fedha nyingi katika miradi hii kwa lengo la kupeleka mbele maendeleo ya nchi na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,**

Uzoefu unaonesha kuwa, miradi mingi inayotekelezwa katika taasisi zetu haiendani na thamani halisi ya fedha, haikamiliki kwa wakati, hali inayopelekea miradi hiyo kukabidhiwa bila ya kuwa na kiwango na baada ya muda mfupi miradi hiyo hupoteza uhalisia wake na kuitia hasara Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mnasaba huu, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Kwanza iweke utaratibu maalumu wa kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi yenyewe na pili, kabla ya kukabidhiwa miradi hiyo ni vyema Wizara ikajiridhisha juu ya utekelezaji wake ili kuepusha hasara zinazoweza kujitokeza baadae na tija ya miradi hii iweze kuwa endelevu kwa kizazi kijacho.

**Mheshimiwa Spika,**

Miradi katika taasisi zetu ni muhimu ikatekelezwa kwa umakini mkubwa hasa tukizingatia miradi hii inatumia gharama kubwa ya fedha katika utekelezaji wake.

## HITIMISHO

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena wewe binafsi **Mheshimiwa Spika,** kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa niaba ya Kamati, pamoja na kuwashukuru wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kutenga muda wao na kunisikiliza kwa umakini wakati nikiwasilisha hutuba hii. Sasa wakati umefika niwaombe wajumbe wa Baraza lako waijadili na kuichangia hotuba hii kwa mustakbali wa taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ninayoiongoza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maelezo hayo, naomba kuwasilisha.

**Ahsante,**

……………………………

Mhe.Yussuf Hassan Idd.
Mwenyekiti,
Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii
Baraza la Wawakilishi
**Zanzibar.**